**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# TANGAZO LA MWALIKO WA TAASISI NA ASASI ZA KIRAIA ZENYE NIA YA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA KATIKA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO LA PERAMIHO, HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA, MKOA WA RUVUMA NA UDIWANI KATIKA KATA YA SHIWINGA ILIYOPO JIMBO LA MBOZI, HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI, MKOA WA SONGWE

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Peramiho lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Mkoa wa Ruvuma na Udiwani katika Kata ya Shiwinga iliyopo Jimbo la Mbozi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Mkoa wa Songwe. Uchaguzi huo utafanyika siku ya Alhamisi tarehe 26 Februari, 2026 katika jimbo na kata tajwa.

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 10(1)(g) na (h) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024 na kanuni ya 22 na 23 za Kanuni za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi za Mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatoa mwaliko kwa taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura katika uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Peramiho na Udiwani katika Kata ya Shiwinga.

Hivyo, kupitia tangazo hili, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inakaribisha maombi kutoka kwa taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu hiyo.

Taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura kuwasilisha maombi yao kupitia kiunganishi (*link*) kifuatacho *https://ams.inec.go.tz* katika Mfumo wa Kusajili Waangalizi, Asasi za Kiraia na Vyombo vya Habari (Accreditation Management System - AMS).

Taasisi au asasi ya kiraia itakayoomba inapaswa kuwa na vigezo vifuatavyo:-

(i) iwe imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania;

(ii) iwe imefanya kazi nchini kwa kipindi kisichopungua miezi sita tangu kusajiliwa kwake;

(iii) ikiwa taasisi au asasi ya kiraia inahusisha watendaji wa kimataifa, miongoni mwa watendaji wake wakuu watatu, wawili wawe Watanzania;

(iv) katika utendaji wake, iwe haijahusishwa na uchochezi au kuvuruga amani;

(v) iwe na uzoefu wa kutoa elimu ya mpiga kura; na

(vi) iwe tayari kujigharamia katika kutoa elimu ya mpiga kura.

Aidha, taasisi au asasi ya kiraia itakapowasilisha maombi katika mfumo, inatakiwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) kuambatisha nakala au kivuli cha cheti cha usajili;

(ii) kuambatisha nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi husika;

(iii) kujaza majina matatu ya viongozi wa juu wa taasisi au asasi husika; na

(iv) kujaza anuani kamili ya makazi na namba za simu za ofisi na za viongozi wake.

Maombi hayo yatapokelewa kuanzia **tarehe 20 Januari, 2026 hadi 26 Januari, 2026.**

**Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha au rasilimali nyingine kwa ajili ya kugharamia zoezi la utoaji wa elimu ya mpiga kura kwa taasisi au asasi za kiraia zitakazopewa kibali.**

**Aidha, maombi yatakayotumwa kwa njia tofauti na mfumo ulioainishwa katika tangazo hili hayatafanyiwa kazi.**

Limetolewa leo tarehe **19 Januari, 2026** na:

Kailima, R. K
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**